BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Thelathini – Tarehe 10 Juni, 2026
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

281. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

(a) Je, Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zipo ngapi na zinatekeleza majukumu gani.

(b) Je, ni sifa zipi zinazohitajika kwa mtu anayetaka kujiunga na vikosi hivyo.

### Wizara ya Fedha na Mipango:

515. MHESHIMIWA ABDULLAH KAMBOTWE ABDULLAH (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

(a) Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) imewekeza kiasi gani katika miradi mbalimbali na mrejesho (return on investment) upoje kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita.

(b) Kwa nini taarifa hizi hazichapishwi kwa uwazi katika magazeti, ili wanachama waweze kupima ufanisi wa Mfuko wao.

**Wizara ya Kazi na Uwekezaji:**

166. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Taratibu za uwekezaji katika nchi yetu ya Zanzibar zinawataka wawekezaji wote kutoka nje ya nchi wanaokuja kuwekeza Zanzibar, kutoa huduma kwa jamii inayowazunguka kwenye maeneo waliyoyaekeza, lakini takribani maeneo mengi ndani ya Zanzibar yamegubikwa na utata wa upatikanaji wa huduma hizo.

(a) Je, ni kiasi gani mpaka sasa kimetolewa na wawekezaji na ni katika maeneo yepi hapa Zanzibar yaliyofaidika kupata fedha hizo kutokana na uwekezaji uliofanywa (Corporate Social Responsibility).

(b) Ni lini Serikali itafika katika kijiji cha Wambaa kwa Azzan jimbo la Chambani kuja kutoa elimu kwa wakaazi wa eneo hilo ili waweze kuzisimamia fedha ipasavyo.

(c) Kwa nini Serikali haifanyii marekebisho sheria husika, ili iwe na nguvu za kuwasimamia wawekezaji wasiotoa huduma au fedha hizo kwa jamii.

149. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi na Uwekezaji:

Kwa kuwa Serikali inaendelea kuitangaza Zanzibar kwa lengo la kuwavutia wawekezaji wengi zaidi, Je, Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha uwekezaji huo hauleti faida kwa wawekezaji pekee bali unaleta maendeleo ya kweli kwa wananchi wa kawaida.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

513. MHESHIMIWA ABDULLAH KAMBOTWE ABDULLAH (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Walimu wengi husasani wa Skuli Binafsi (Private Schools), wamekuwa wakiajiriwa kinyume na utaratibu na wengi wao wanafanya kazi pasipokuwa na mikataba, huku waajiri wengi wanawasimamisha kazi kinyume na utaratibu na kuwanyima haki zao za msingi.

Je, Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha kuwa walimu hao

wanapata haki zao za msingi na kuwa na uhakika na ajira zao.

526. MHESHIMIWA SAID ALI JUMA (Uteuzi wa Rais) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Pamoja na juhudi za Serikali ya Awamu ya Nane za kuboresha miundombinu ya elimu nchini kote, bado kuna changamoto ya skuli kukosa uzio.

Je, Serikali imejipangaje kutatua changamoto ya skuli kukosa uzio

## Wizara ya Afya:

162. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Je, Serikali inasimamia vipi ubora wa huduma za afya zinazotolewa na Hospitali Binafsi ili kulinda haki za wagonjwa.

291. MHESHIMIWA ALLEY MASOUD ALLEY (Jimbo la Mtambile) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa wananchi hawapati taarifa yoyote kuhusu ugonjwa wa UKIMWI.

(a) Je, maradhi haya hayapo tena hapa Zanzibar.

(b) Na kama yapo, ni hatua gani Serikali imezichukua kuwafahamisha wananchi, ili kulinda nguvu kazi ya Taifa na kuzuia janga hilo.

## Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

527. MHESHIMIWA SAID ALI JUMA (Uteuzi wa Rais) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Tumeshuhudia Serikali ya Awamu ya Nane imechukua jitihada kubwa ya kuboresha miundombinu ya barabara, kwa kujenga Barabara Kuu na Barabara za Ndani kwa kiwango cha lami, mpaka Mji wetu umekuwa kama kiganja. Hata hivyo, Serikali ilipata tabu wakati wa ujenzi wa barabara hizo kutokana na watu kujenga kiholela, kulikosababishwa kwa kiasi kikubwa na wananachi wenye maeneo kuendelea kukata na kuuza viwanja katika maeneo yao bila ya kufuata utaratibu.

Je, Serikali imejipangaje kuongoza wananchi wanaouza viwanja

bila ya utaratibu.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

221. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Vita na mapigano mbalimbali yanayoendelea duniani, ikiwa ni pamoja na vita vya Urusi na Ukraine na vita vya Israel na Marekani dhidi ya Irani vina athari kubwa kwa nchi yetu.

(a) Je, Serikali inasimamia vipi upatikanaji wa mafuta ya petroli, diseli na mafuta ya ndege, kwa wananchi wake.

(b) Je, kuna athari yoyote ya ongezeko la bei ya mafuta hayo kwa wananchi kutokana na uwepo wa vita hivyo.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

379. MHESHIMIWA DKT. MAHMOUD OMAR HAMAD (Jimbo la Tumbatu) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Ni lini Serikali itakamilisha marekebisho ya Sheria za Mtoto ili iendane na mahitaji ya sasa.

380. MHESHIMIWA DKT. MAHMOUD OMAR HAMAD (Jimbo la Tumbatu) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha vituo vya malezi na makaazi ya watoto yatima na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi.

**Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:**

76. MHESHIMIWA MAHFOUDH ABDALLA MOHAMMED (Jimbo Magomeni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Ujenzi wa kiwanja cha Mpira Mzalendo ni faraja kubwa kwa wananchi wa Magomeni hasa wanamichezo na wadau wa mazoezi. Hata hivyo, dizaini ya ujenzi wa uwanja huo hasa kuupunguza ukubwa wake, ni jambo ambalo halikupokewa vizuri na wanamichezo hao wala wamiliki wa uwanja huo.

(a) Ni ipi kauli ya Serikali kwa waliokuwa wamiliki wa uwanja huo (Timu ya Mzalendo) ya kuendelea kuutumia uwanja huo bure baada ya kukamilika kwake.

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuziendeleza fursa za ujenzi wa viwanja vya michezo kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

190. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:

Zanzibar ni nchi inayotambulika kwa kuzalisha vipaji vingi sana katika michezo ya mpira wa miguu, mpira wa pete, riadha pamoja na michezo mengine mbalimbali.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha vipaji hivyo vinafaidisha Soko la Kimataifa.

(b) Je, Serikali imechukua jitihada gani kuziwezesha *"academy"* zinazowakuza watoto katika michezo kwa upande wa Kisiwa cha Pemba.

(c) Ni upi mpango wa Serikali katika kuhakikisha Ligi Kuu ya Soka ya Zanzibar inastawi na kuongeza hamasa.

## <u>Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:</u>

7. MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Wapo baadhi ya madereva wa bajaji kisiwani Pemba wamezisajili bajaji zao kutoa huduma ya teksi (tax), ambapo zingelitoa huduma ya usafiri kwa abiria kutoka sehemu moja hadi anakofika abiria huyo, lakini badala yake wanafaya kazi kwa nafasi ya daladala kwa maana ya kuchukua abiria kutoka kituo kimoja hadi chengine sawa na zamu (routes) za daladala hizo, matokeo yake daladala zenye 'route' ya kutoka mjini kwenda Wesha, kutoka mjini kwenda Vitongoji, kutoka mjini kwenda Gombani na kutoka Wete kwenda Gando, zimepungua sana na kuelekea kumalizika kabisa.

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya hali hii.

310. MHESHIMIWA MAHFOUDH ABDALLA MOHAMMED (Jimbo Magomeni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Barabara za ndani zinazojengwa katika jimbo la Magomeni ni nyembamba sana ambazo haziruhusu kupishana gari, hivyo matumizi yake ni ya *single way*.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara za pembeni yake hasa katika barabara za Najim – Mtumwajeni na Mea – Magomeni, ili zitumike sambamba na hizo za *single way* na kuwa *'in and out'*.

**<u>Wizara ya Biashara na Maendelo ya Viwanda:</u>**

318. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendelo ya Viwanda:

Kumekuwepo na ongezeko la uingizaji wa vifaa vilivyotumika kutoka nje ya nchi kwa ajili ya kuuzwa katika soko la ndani, hali inayoweza kuhatarisha usalama wa watumiaji na kuathiri ubora wa bidhaa zinazotumika na wananchi.

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha udhibiti wa ubora wa bidhaa zilizotumika zinazoingizwa nchini ili kuhakikisha zinakidhi viwango vya usalama na ubora unaotakiwa.

(b) Je, ni hatua gani zimechukuliwa kudhibiti uingizaji na uuzaji wa vifaa chakavu vinavyoweza kuhatarisha watumiaji.

**<u>Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:</u>**

447. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Kumekuwa na matukio mbalimbali kwenye Mitandao ya Kijamii kwa kutumika vibaya na kuchafua taaswira na maadili ya jamii na kukashifu.

Ni hatua zipi zinazochukuliwa dhidi ya wahusika wanaotumia Mitandao ya Kijamii kwa kuwadhalilisha wanawake hasa katika maeneo ya faragha na maeneo ya mikusanyiko ya watu kama vile masokoni.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

356. MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (Jimbo la Ole) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kuwa Mji Mkongwe ni Taasisi yenye kujitegemea, yenye haki ya kushitaki na kushitakiwa.

(a) Je, ni kesi ngapi ambazo Mamlaka ya Mji Mkongwe imeshitakiwa mpaka sasa.

(b) Je, ni mashauri mangapi yameamuliwa Mahakamani na mangapi Mamlaka imeshinda.

(c) Je, mpaka sasa Mamlaka imetakiwa kulipa kiasi gani kutokana na mashauri iliyoshindwa Mahakamani.

**Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji:**

450. MHESHIMIWA JUMA HASSAN THABIT (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Ajira na Uwezeshaji:

Licha ya jitihada mbalimbali za Serikali katika kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia Taasisi ya ZEEA, bado kuna changamoto ya upatikanaji wa mikopo kwa wananchi hususani wakaazi wa Jimbo la Fuoni.

(a) Ni idadi gani ya wanachi wa Jimbo la Fuoni waliofaidika na mikopo hiyo.

(b) Ni lini Serikali itaweka vigezo vya upatikanaji wa mikopo hadharani, ili kuweza kuondoa utata wa upatikanaji wa mikopo hiyo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

467. MHESHIMIWA MAKAME MOHAMED SUFIANI (Jimbo la Muembemakumbi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Matayarisho ya matengenezo ya Boti za Uvuvi (Fibers) zilizogaiwa kwa Wavuvi katika kipindi cha awamu ya mwanzo, hayakuhusisha maoni na mahitaji ya Wavuvi ambao ndio watumiaji. Jambo hili lilipelekea baadhi boti hizo (fiber) kukosa vigezo vya mahitaji ya wavuvi.

Je, katika awamu ijayo itawahusisha vipi watumiaji (Wavuvi), ili kuepuka changamoto zilizojitokeza awali.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

258. MHESHIMIWA KHAMIS MOHAMMED AMRAN (Jimbo la Mkoani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kumekua na changamoto kubwa ya Majaji wa Mahakama Kuu upande wa Zanzibar, hali inayopelekea kuzorota kwa utoaji wa huduma na ucheleweshaji wa kesi.

(a) Je, kuna Majaji wangapi wa kudumu wa Mahakama Kuu wanaotoa huduma Kisiwani Pemba.

(b) Serikali ina mkakati gani wa kuongeza idadi ya Majaji wa Mahakama Kuu ambao watakuwa wanatoa huduma kisiwani Pemba, ili kuondoa changamoto ya ucheleweshaji wa kesi kwa wananchi.

**Zanzibar,**
**10 Juni, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**WAWAKILISHI, ZANZIBAR**